

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



16 MEI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA ISHIRINI NA TATU – TAREHE 16 MEI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WIZARA YA KILIMO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WIZARA YA AFYA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

197. MHESHIMIWA SALMA RASHID KIKWETE (MCHINGA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itafanya ukarabati mkubwa katika Shule ya Msingi Kingurungundwa iliyopo Mchinga.

198. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itaigawa Jimbo la Mbarali na kuwa na Halmashauri mbili ili kusogeza huduma karibu na Wananchi.

WIZARA YA MAJI:

199. MHESHIMIWA MARYAM AZAN MWINYI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakomesha shughuli za ukataji miti, kilimo na ujenzi karibu na vyanzo vya maji ili kulinda vyanzo hivyo.

WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:

200. MHESHIMIWA MOHAMED LUJUO MONNI (CHEMBA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:-

Je, ni lini Serikali itamalizia ujenzi wa Kituo cha Polisi cha Wilaya ya Chemba uliokwama kwenye ngazi ya lenta kwa miaka mitatu sasa.

WIZARA YA MALIASILI NA UTALII:

**201. MHESHIMIWA PRISCUS JACOB TARIMO
(MOSHI MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maliasili na Utalii:-

Je, kuna mpango gani wa kusaidia Halmashauri zinazozunguka Mbuga na Hifadhi kwa kutoa CSR kwenye mapato ya utalii.

WIZARA YA AFYA:

**202. MHESHIMIWA HAWA SUBIRA MWAIFUNGA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, ni lini Serikali itatatua changamoto ya vifaa vya kufundishia na uhaba wa Wakufunzi katika Chuo cha Afya kilichopo Hospitali ya Kitete.

**203. MHESHIMIWA KHADIJA SHAABAN TAYA
(VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:-

Je, Serikali kwa kushirikiana na Wahisani ina mpango gani mahsusi wa kutoa bima za afya bure kwa Watu wenye Ulemavu wa kudumu.

WIZARA YA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI:

204. MHESHIMIWA USSI SALUM PONDEZA (CHUMBUNI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki:-

Je, ni nchi ngapi zimeshafungua Ofisi zao za Ubalozi Jijini Dodoma baada ya zoezi la kuhamisha Makao Mkuu ya Serikali Dodoma.

WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

205. MHESHIMIWA VITA RASHID KAWAWA (NAMTUMBO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, mpango wa ujenzi wa reli ya kusini kutoka Mtwara hadi Ruvuma na matawi yake ya Liganga na Mchuchuma umefikia wapi.


206. MHESHIMIWA ALI JUMA MOHAMED (SHAURIMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

- Je, Shirika la Ndege nchini (ATCL) limeshaanza kulipa madeni ya Makampuni yaliyokuwa yanatoa huduma.



IV. HOJA ZA SERIKALI:



WAZIRI WA AFYA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Afya kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA
16 MEI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**